**“Mtakuwa Watakatifu Kwa Kuwa Mimi Ni Mtakatifu” 1 Petro 1:16**

Hivi umewahi kutulia ukaitafakari aya hii na kukaa juu ya kile ambacho Petro anajaribu kutueleza. Anatuamuru kuwa “watakatifu,” kama Mungu mwenyewe alivyo Mtakatifu. Hii ndiyo jumla ambayo ni rahisi kusema, kuongea, kufikiri na kukubali. Si ndiyo? Ni tofauti kabisa na uhalisia wa kuwa watakatifu kama yeye alivyo mtakatifu.

1 Petro 1:16 inaanza kwa kusema, “Kwa maana imeandikwa.” Nukuu hii ambayo Petro amechukua inatoka katika maandiko ya Musa katika Mambo ya walawi. Katika Mambo ya Walawi 11:44; 20:7, na 26, Musa anawaamuru wana wa Israeli kuwa watakatifu kama Mungu alivyo mtakatifu. Yesu aliikaza amri hii katika Mathayo 5:48, alipotuambia tuwe wakamilifu, hapa napo,ni  jumla iliyo rahisi kusema lakini ngumu kutekeleza.

Natambua ya kuwa aya hii kwa mara ya kwanza ilikusudiwa kwa Wana wa Israeli. Kimsingi, misingi yetu iko sawa na wao, kwa sababu wana wa Israeli wa kale na Wakristo sote tunakiri ya kwamba tu watu wake. Kama tunashiriki ungamo la aina moja na wale wa zamani, basi, “Mataifa yote watakwenda kila mmoja kwa jina la mungu wake, na sisi tutakwenda kwa jina la BWANA, Mungu wetu, milele.” Mika 4:5

Hivyo, tunawezaje kuenenda ili tuwe watakatifu kama yeye alivyo? Ni lazima:
Tujiepushe na unajisi
Tujitenge na ulimwengu
Alifanyalo tulichukulie kuwa sahihi
Tutafute kuiga utakatifu wake
Tabia yetu ifananishe na yake
Na tuufurahie uso wake

Naam, Naam, najua hugharimu mengi ili kuwa mtakatifu. Na natambua kuwa ukamilifu haumo ndani yetu. Walakini blogu yetu hii itajikita katika dhana ya “Kuwa Wataktifu.”

Kama ungependa kutoa mawazo mawili matatu hapa na pale, yatume kwangu kwa njia ya barua pepe, nami nitayaweka. Maana tunahitaji kila msaada unaoweza kupatikana ili tuwe watakatifu kama yeye ALIVYO!

Amani tele.